# KUZUIA UKATILI DHIDI YA WATOTO



# Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania na Mpango wa Kitaifa wa Kudhibiti

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

ACHA! Ukatili kwa watoto
WALINDE

## Usuli

Baada ya kuchapishwa kwa *Ripoti ya Dunia ya Ukatili Dhidi ya Watoto* ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa iliyotolewa mwaka 2006, pendekezo maalumu lilitolewa la kutayarisha na kutekeleza ukusanyaji wa data na kufanya utafiti wa ukatili dhidi ya watoto katika ngazi ya taifa.



Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeitikia wito huo wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa kuwa nchi ya kwanza katika bara la Afrika, kufanya utafiti ulioshirikisha sampuli ya watu kitaifa ili kutathmini juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto, kwa kupima aina zote za ukatili (kijinsia, kimwili, na kiakili) dhidi ya vijana wa kike na wa kiume.

Utafiti Kuhusu Ukatili Dhidi ya Watoto ulifadhiliwa na UNICEF mwaka 2008 na kuratibiwa na timu ya watafiti kutoka Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa Altanta, na Chuo Kikuu Shirikishi cha Afya na Sayansi ya Tiba cha Muhimbili Dar es Salaam.

## Kikosi Kazi Kinachojumuisha Sekta mbalimbali

*Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania* (UUDWT) umeongozwa na Kikosi Kazi cha Kitaifa ambacho kimejumuisha sekta mbali mbali chini ya uenyekiti wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kikosi Kazi cha Kisekta kilihusisha wajumbe kutoka sekta za umma na binafsi, ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa serikali kutoka Wizara ya Elimu, Afya na Ustawi wa Jamii, Sheria na Polisi, TACAIDS, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, taasisi na wadau wa maendeleo.

Kuanzishwa kwa kikosi hiki kitaifa cha uratibu kimesaidia kuongoza utafiti, pamoja na utekelezaji wake na utayarishaji wa ripoti ya mwisho. Pia kimesaidia kuufanya utafiti huu kuwa wa kitaifa na kuupeleka utafiti huu kwenye vitendo.

## Matokeo

### *Ukatili wa kijinsia uliotokea utotoni*

**Kiwango cha ukatili wa kijinsia ni kikubwa:** wasichana 3 kati ya 10 na mvulana 1 kati ya 7 wanasema walifanyiwa ukatili wa kijinsia kabla ya kufikisha miaka 18. Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita asilimia 6 ya wavulana Tanzania wenye umri kati ya miaka 13 hadi 17 wanasema walifanyiwa tukio moja la ukatili wa kijinsia. Kiwango cha ukatili wa kijinsia kwa wasichana wa Kitanzania ni mara mbili zaidi asilimia 14. Zaidi ya asilimia 6 ya wasichana wenye umri kati ya miaka 13 hadi 24 ambao walipata mimba wanasema angalau ujauzito mmoja ulitokana na kufanyiwa ukatili wa kijinsia.

**Ukatili wa kijinsia ulifanyika mara nyingi:** Kati ya waathirika wa ukatili wa kijinsia, takriban wasichana 4 kati ya 10 na wanaume 3 kati ya 10 wanasema walifanyiwa ukatili wa kijinsia mara tatu au zaidi kabla ya kufikisha miaka 18.

**Kushikwa bila ridhaa au kutomasa na jaribio la kufanya ngono ndio udhalilishaji uliofanywa mara nyingi:** Wasichana na wavulana Tanzania wanasema kushikwa bila ridhaa au kutomasa ndio ukatili wa kijinsia unaoongoza ukifuatiwa na jaribio la kufanya ngono. Asilimia 6.9 ya wasichana na asilimia 2.9 ya wavulana walilazimishwa au walishurutishwa kufanya ngono kabla ya kufikisha umri wa miaka 18.

**Ngono ya mara ya kwanza ilikuwa bila ridhaa:** Asilimia 18 ya wavulana Tanzania na asilimia 29 ya wasichana ambao walifanya ngono kabla ya kufikisha miaka 18 walisema tukio la kwanza lilikuwa sio kwa ridhaa yao.

**Waathirika ni wa rika zote:** Ukatili wa kijinsia unawaathiri watoto wa rika zote. Takriban asilimia 20 ya wasichana wanasema kuwa walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa mara ya kwanza wakiwa na umri chini ya miaka 14; asilimia 40 ya wasichana walifanyiwa ukatili wa kijinsia kwa mara ya kwanza wakiwa na umri kati ya miaka 14 na 15; na asilimia nyingine 40 ya wasichana walifanyiwa ukatili wa kijinsia wakiwa na umri wa kati ya miaka 16 na 17. Kwa wavulana, asilimia 16 walifanyiwa ukatili wa kijinsia kwa mara ya kwanza wakiwa na umri chini ya miaka 14; asilimia 27 walikuwa na umri kati ya miaka 14 na 15; na Takriban asilimia 60 wakiwa na umri wa miaka kati ya 16 na 17.



Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

**Matumizi ya nguvu ni jambo la kawaida:** Takriban nusu ya wavulana wa Tanzania, na wasichana 7 kati ya 10 wanasema nguvu au vitisho vilitumika katika kujaribu au kuwalazimisha kufanya ngono. Asilimia 28 ya wasichana na asilimia 19 ya wavulana walisema wahusika walitumia uongo, hila au unyanyasaji katika kutimiza azma zao.

**Matukio mengi ya ukatili hufanyika majumbani au shuleni:** Takriban nusu ya matukio ya ukatili wa kijinsia yalifanyika katika majumba ya watu, hii inaendana na taarifa kuwa wahusika ni watu ambao waathirika wanawafahamu. Asilimia 45 ya wasichana walifanyiwa tukio moja la kutomasa, au jaribio la ngono wakiwa majumbani mwao. Wasichana ndio walioko katika hali hatarishi zaidi ya kufanyiwa ukatili, walisema angalau tukio moja la kutomasa au jaribio la ngono lilitokea wakiwa katika mazingira ya shule asilimia 17, na asilimia 26 walifanyiwa ukatili huo wakati wakitoka au kwenda shule. Takriban robo ya wasichana, sawa na asilimia 24.2, wanasema tukio angalau moja la ukatili wa kijinsia lilifanyikia porini, mtoni au kando kando ya barabara, na asilimia 10 walisema walifanyiwa ukatili wa kijinsia katika sehemu za jamii mfano sehemu za biashara au baa. Kwa wavulana zaidi ya robo, yaani asilimia 26.7 walisema tukio angalau moja la ukatili wa kijinsia lilifanyika shambani, kichakani, mtoni au kando kando ya barabara.

**Watoto wanawafahamu wanaowafanyia ukatili wa kijinsia:** Kwa wasichana, takriban theluthi moja walisema kuwa tukio angalau moja la ukatili wa kijinsia lilifanywa na jirani; theluthi nyingine moja walisema kuwa walifanyiwa ukatili huo na watu wasiowafahamu, na robo ya wasichana wanasema walifanyiwa ukatili wa kijinsia na wapenzi wao. Takriban msichana 1 kati ya wasichana 10 walisema angalau mhusika mmoja wa ukatili wa kijinsia alikuwa mwalimu, wakati ambapo asilimia 7 walisema ukatili wa kijinsia dhidi yao ulifanywa na ndugu—hasa mjomba au binamu. Mvulana 1 kati ya 2 ambao walifanyiwa ukatili wa kijinsia wanasema kuwa angalau mhusika mmoja wa ukatili huo alikuwa ni mpenzi, wakati ambapo robo wanasema walifanyiwa ukatili huo na watu wasiowafahamu.

**Matukio mengi ya ukatili wa kingono yalifanyika mchana kweupe:** Matukio mengi ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wasichana na wavulana yalifanywa kati ya adhuhuri na saa 2 usiku. Asilimia 43.4 ya wasichana na asilimia 35.4 ya wavulana walisema angalau tukio moja la ukatili wa Kijinsia lilifanyika kati ya adhuhuri na saa 11 jioni. Zaidi ya theluthi moja ya wasichana na wavulana wanasema tukio la ukatili wa kijinsia lilifanyika kati ya saa 11 jioni na saa 2 usiku. Ni wavulana na wasichana wachache waliosema kuwa walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kati ya usiku wa manane na saa 1 asubuhi.

**Watoto wengi hawatoi taarifa kuhusu udhalilishaji wa kijinsia:** Takriban nusu ya wasichana na theluthi 2 ya wavulana hawamwambii mtu yeyote kuhusu ukatili wanaofanyiwa. Zaidi ya asilimia 60 ya wasichana wanasema sababu za kifamilia na kijamii ndizo hasa zinazowafanya wasiwambie watu (sababu kubwa ni uoga wa kutengwa au kusambaratisha familia). Asilimia nyingine 26 wanasema hawakutoa taarifa kwa sababu zao binafsi. Kwa wavulana, asilimia 58 wanasema hawakutoa taarifa kwa sababu zao binafsi (sababu kubwa ni kwamba hawadhani ni tatizo kubwa sana), wakati ambapo asilimia 36 wanasema sababu za kifamilia na kijamii ndizo zilizowafanya wasitoe taarifa. Asilimia 41 ya wasichana walimwambia mzazi na asilimia 36 walimwambia rafiki, wakati ambapo asilimia 71 ya wavulana waliwaambia rafiki zao.

**Watoto wachache wanatafuta huduma, na wachache mno wanazipata:** Msichana mmoja tu kati ya 5 na mvulana 1 kati ya 10 wanatafuta huduma baada ya kufanyiwa ukatili. Kati ya hao, msichana mmoja kati ya 10 na mvulana mmoja kati 25 waliokumbwa na ukatili wa kijinsia walipata huduma. Takriban asilimia 16 ya wasichana na wavulana wangependa kupata huduma za ziada kama ushauri nasaha, huduma za kipolisi au msaada kutoka ustawi wa jamii.

## *Ukatili wa kimwili uliotokea utotoni*

**Kiwango cha ukatili wa kimwil kiko juu kuliko ukatili wa kijinsia:** Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, zaidi ya nusu ya wavulana na wasichana Tanzania wamefanyiwa ukatili wa kimwili kama vile kupigwa ngumi, makofi, kuchapwa fimbo, kupigwa teke, au kutishiwa na silaha kama bunduki au kisu. Katika kipindi cha utoto, takriban robo tatu, asilimia 72 ya wasichana na asilimia 71 ya wavulana walifanyiwa ukatili wa kimwili kabla hawajafikisha umri wa miaka 18.

**Watoto wanafanyiwa ukatili wa kupigwa na wazazi na walimu:** Takriban asilimia 60 ya wasichana na wavulana wa Tanzania ambao walitoa taarifa ya kufanyiwa ukatili wa kimwili (kupigwa ngumi, kuchapwa fimbo au kupigwa teke), wanasema walifanyiwa ukatili huo na ndugu, baba na mama wakiwa wahusika wakubwa. Kiwango cha ukatili wa kimwili kinachofanywa na walimu ni kikubwa sana -asilimia 52.6 ya wasichana na asilimia 50.8 ya wavulana walifanyiwa ukatili wa kimwili na walimu kabla ya kufikisha umri wa miaka 18.

**Udhalilishaji hufanyika majumbani na shuleni:** Asilimia 46 ya wasichana na wavulana wa Kitanzania ambao walifanyiwa ukatili wanasema walipigwa ngumi, mateke au kuchapwa viboko angalau mara tano na ndugu zao kabla ya kufikisha umri

wa miaka 18. Takriban theluthi moja walifanyiwa ukatili wa kimwili angalau mara moja au mbili wakati wakiwa watoto wadogo. Ukatili wa kimwili unaofanywa na walimu pia ni wa kiwango kikubwa: Asilimia 78 ya wasichana na asilimia 67 ya wavulana ambao walifanyiwa ukatili na walimu wao, wanasema walipigwa ngumi, mateke au kuchapwa viboko zaidi ya mara tano kabla ya kufikisha umri wa miaka 18.

## *Ukatili wa kiakili uliotokea utotoni*

**Robo ya watoto wamefanyiwa ukatili wa kiakili:** Takriban robo ya watoto wa Tanzania wanafanyiwa ukatili wa kiakili, kama vile kuitwa majina mabaya ndio tabia iliyozoeleka, yaani asilimia 22 ya wavulana na asilimia 18 ya wasichana walitoa taarifa za kufanyiwa ukatili wa kiakili. Takriban asilimia 9 ya wasichana hujihisi kama hawatakiwi, wakati ambapo asilimia 4 wanatishiwa kutengwa. Zaidi ya asilimia 7 ya wavulana wanahisi kutotakiwa, na takriban asilimia 5 wanatishiwa kutengwa.

**Ndugu na majirani wanashiriki katika ukatili wa kiakili:** Takriban asilimia 80 ya wasichana wa Kitanzania na asilimia 65 ya wavulana ambao walifanyiwa ukatili wa kiakili wanasema walifanyiwa ukatili huo na ndugu. Asilimia 20 ya wasichana na asilimia 34 ya wavulana Tanzania wanasema walifanyiwa ukatili wa kiakili na majirani. Watoto wanaofanyiwa ukatili wa kiakili wanafanyiwa na watu wengi: Asilimia 42 ya wasichana wa Tanzania na asilimia 38 ya wavulana wanasema walifanyiwa ukatili huo na mtu zaidi ya mmoja.

## *Watoto hufanyiwa aina nyingi za ukatili – watoto wengi wanakumbwa na aina nyingi za hali hatarishi*

Muingiliano na mahusiano baina ya aina tatu za ukatili dhidi ya watoto zinadhihirisha wazi aina nyingi za hali hatarishi zinazowakabili watoto wa Tanzania. Zaidi ya wasichana 8 kati ya 10 ambao walifanyiwa ukatili wa kijinsia pia walifanyiwa ukatili wa kiakili, wakati ambapo zaidi ya watoto 4 kati ya 10 pia waliofanyiwa ukatili wa kiakili ilikuwa ni pamoja na ukatili wa kimwili na kijinsia. Kwa wavulana waliofanyiwa ukatili, 8 kati ya 10 pia waliofanyiwa ukatili wa kimwili; na 5 kati ya 10 waliofanyiwa ukatili wa kiakili ilikuwa ni pamoja na ukatili wa kijinsia na kimwili.

## *Yatima wako kwenye hali hatarishi zaidi*

Watoto yatima wanakuwa kwenye hatari zaidi ya kufanyiwa ukatili kuliko watoto wasio yatima. Asilimia 36 ya watoto yatima walifanyiwa ukatili wa kijinsia kabla ya kufikisha umri wa miaka 18, ikilinganishwa na asilimia 25 ya wasichana ambao si yatima, wakati asilimia 31 ya watoto yatima walifanyiwa ukatili wa kiakili walipokuwa wadogo, ikilinganishwa na asilimia 21 ya wasichana ambao si yatima. Wavulana ambao walifiwa na mama zao kabla ya kufikisha miaka 18 walifanyiwa vitendo vingi vya ukatili wa kiakili kuliko wale ambao hawakufiwa na mama zao (asilimia 44 ya yatima ikilingashwa na asilimia 26 ya wavulana ambao si yatima).

## *Madhara ya kiafya yanayosababishwa na ukatili dhidi ya watoto*

Matatizo mengi ya kiafya na kitabia yanayotokea wakati wa ujana na wakati wa utu uzima yana uhusiano na ukatili uliofanywa utotoni. Hususan, Ukatili wa kijinsia, unahusiana na ongezeko la hatari ya kupata matatizo ya afya ya uzazi, pamoja na maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi pamoja na magonjwa mengine ya zinaa. Tafiti zilizopita zinazohusisha ukatili dhidi ya watoto na matatizo ya kiafya, zikijumuishwa na matokeo ya utafiti huu, zinaonyesha kuwa kupunguza ukatili dhidi ya watoto kutapunguza matatizo ya afya na gharama za matibabu ya afya ya kimwili na kiakili miongoni mwa watu.

**Udhalilishaji wa kijinsia unahusiana na tabia hatarishi:** Matumizi ya kondomu Tanzania ni kidogo sana miongoni mwa wanawake na wanaume waliofanyiwa ukatili wa kijinsia utotoni ukilinganisha na wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo: Asilimia 46 ya wanawake waliofanyiwa ukatili wanasema hawatumii kondomu ikilinganishwa na asilimia 24 ya wanawake ambao hawakufanyiwa ukatili wa kijinsia; Asilimia 57 ya wavulana Tanzania waliofanyiwa ukatili wa kijinsia hawatumii kondomu ikilinganishwa na asilimia 30 ya wanaume ambao hawakufanyiwa ukatili huo. Wanawake na wanaume waliofanyiwa ukatili wa kijinsia utotoni wana uwezekano mkubwa wa kuwa na wapenzi wengi kuliko wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo. Biashara ya ngono ilidhihirika zaidi miongoni mwa wasichana ambao walifanyiwa ukatili wa kijinsia utotoni, kuliko wale ambao hawakuwa na hstoria ya ukatili wa kijinsia utotoni.

**Ukatili wa kijinsia hauathiri tabia ya kupima virusi vya ukimwi:** Wanawake na wanaume ambao wamefanyiwa ukatili wa kijinsia hawakuwa na ufahamu wa sehemu za kupimia virusi vya ukimwi sawa na wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo. Hali kadhalika, kiwango cha upimaji virusi vya ukimwi kwa wale ambao wamefanyiwa ukatili wa kijinsia kinalingana na kiwango cha upimaji wa virusi vya ukimwi kwa wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo.

**Ukatili wa kijinsia na kimwili unahusiana na afya mbaya ya wanawake:** Wanawake wa Tanzania ambao wamefanyiwa ukatili wa kijinsia wana uwezekano mkubwa wa kuwa na msongo wa mawazo, hali ya kuwa na kiwewe, kupata magonjwa ya zinaa na kunywa pombe ikilinganishwa na wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo. Hali kadhalika wanawake ambao wamefanyiwa ukatili wa kimwili wana uwezekano wa kuwa na afya mbaya, kuwa na kiwewe na kuwa na mawazo ya kujiua kuliko wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo.

**Ukatili wa kiakili unawaathiri wanawake na wanaume Tanzania:** Wanaume na wanawake ambao wamefanyiwa ukatili wa kiakili wana uwezekano mkubwa wa kuathirika kiafya, kuwa na msongo wa mawazo, kuwa na kiwewe na kuwa na mawazo ya kujiua. Hali kadhalika wanaume waliofanyiwa ukatili wa kiakili wana uwezekano wa kunywa pombe ikilinganishwa na wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo.

## Mpango wa Kazi Kitaifa wa Kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto Tanzania

### *Ushirikishwaji wa sekta mbalimbali*

Kuwalinda watoto dhidi ya ukatili na udhalilishaji kunahitaji kushirikisha sekta mbali mbali. Chini ya uongozi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Kikosi kazi kinachojumuisha sekta mbali mbali kinatoa mapendekezo yanayolenga sekta husika zikiwemo: sheria na polisi, afya, elimu, ustawi wa jamii, asasi za kiraia, jamii na wana habari. Hakuna sekta moja au taasisi yenye ujuzi, maarifa na raslimali za kutosha kukidhi mahitaji yote ya kumlinda mtoto. Kwa hiyo ni muhimu Mpango wa kukabiliana na ukatili unachangiwa na sekta zote na watu wenye kufanya kazi na watoto pamoja na familia zinazohitaji huduma na ulinzi kwa watoto.

Maeneo makubwa ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kukabiliana na Ukatili dhidi ya Watoto ni pamoja na:

- Kuanzishwa na kutumika kwa mfumo wa kisheria utakaosaidia kulinda watoto dhidi ya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji, ambao utaendana sambamba na Sheria ya Mtoto Na 21 (2009).
- Watendaji wanaosimamia utekelezaji wa sheria kama polisi, mahakama na waendesha mashtaka wana uwezo wa kuendesha kesi za waathirika wa ukatili kwa makini na muda unaostahili ili kutoa haki kwa waathirika wa ukatili na udhalilishaji.
- Huduma yenye kujumuisha maswala mengi ya kiafya inatolewa kwa watoto waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji.
- Mahitaji ya watoto kiakili na kimwili ya kiafya yanayohusu uzuiaji wa ukatili, matunzo na matibabu yanaingizwa katika miongozo na taratibu za kitaifa zinazoandaliwa kwa kuzingatia ukatili wa kijinsia katika sekta ya afya.
- Watoto wanakuwa salama shuleni na uongozi wa shule, walimu wakuu na walimu wana uwezo wa kukabiliana na kesi za ulinzi kwa watoto wakishirikiana na wadau wengine wa kitaifa.
- Watoto na familia zinazohitaji huduma za matunzo na ulinzi wanaweza kuzipata na Idara ya Ustawi wa Jamii ina uwezo wa kutoa msaada unaotakiwa na kuratibu mpango wa kuwalinda watoto kitaifa.
- Asasi za kiraia na jamii wanawezeshwa kutambua, kutoa taarifa na kukabiliana na kesi za unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto.
- Huduma za kijamii zinazingatia njia za ulinzi zinazosaidia kujenga tabia ya kutovumilia aina yoyote ya ukatili kwa kushirikisha jamii - wanawake, wanaume na watoto katika kuzuia ukatili na kuelimisha madhara ya ukatili.
- Watoto na watu wazima wana uelewa mkubwa kuhusu masuala ya ukatili na udhalilishaji wa watoto na huduma iliyopo ya kukabiliana na kesi za watoto ambao ni waathirika wa ukatili.
- Mpango wa Kitaifa wa mawasiliano kwa njia ya simu (Child Helpline) unaanzishwa kwa lengo la kuwalinda watoto na kukabili vitisho au matendo ya ukatili wa kiakili, kimwili au kijinsia dhidi ya watoto.

Mafanikio ya kila eneo yatahusisha malengo yaliyopendekezwa katika kila sekta. Ulinzi wa watoto dhidi ya ukatili na udhalilishaji unahitaji mchango wa kila sekta.

**Tuungane kumaliza Ukatili Dhidi ya Watoto**

Wasiliana na TVAC Sekretarieti, UNICEF, S.L.P 4076, Dar es Salaam,
Tanzania au tuma baruapepe kwenda daresalaam@unicef.org